



The United Republic of Tanzania
Prime Minister's Office
National Economic Empowerment Council



12 Kivukoni Front
P.O. Box. 1734 Dar-Es-Salaam
Tel: +255 22 2137362
Tel /fax : +255 22 2125596
Email : nec@uwezes haji.go.tz
Website: www.uwezes haji.go.tz

12 Barabara ya Kivukoni
S.L.P. 1734 Dar-Es-Salaam
Simu: +255 22 2137362
Simu/Nukushi: +255 22 2125596
Barua Pepe : nec@uwezes haji.go.tz
Tovuti : www.uwezes haji.go.tz

TAARIFA KWA UMMA

Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) linapenda kuchukua fursa hii kuwatangazia Wadau wote wa Uwezeshaji kutoka kwenye Wizara, Idara, Taasisi za Umma na Sekta Binafsi kuhusu Kongamano la Nne la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ambalo linatarajia kufanyika Tarehe 15 Juni 2019 katika ukumbi wa Hazina mjini Dodoma.

Mgeni rasmi wa Kongamano hili anatarajia kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mh. Kassim Majaliwa Majaliwa (MB) ambaye atazindua ripoti ya mwaka ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na kuwatambua Wadau wa Uwezeshaji waliofanya vizuri kutoka kwenye Wizara, Idara, Taasisi za Umma na Sekta binafsi kwa kuwapa tuzo za vikombe na vyeti.

Kongamano la mwaka huu linabeba ujumbe wa 'Wezesha Watanzania kujenga Viwanda'.

Wakati wa Kongamano kutakuwa na mada mbalimbali zitaibuliwa na waendesha mijadala ili kushirikishana uzoefu katika masuala ya uwezeshaji wananchi na hasa katika eneo la Viwanda.

Baraza linawakaribisha wadau wote wa uwezesaji kuhuduria katika kongamano hili lenye shabaha ya kuhamasisha ushiriki wa Wananchi, sekta za Umma na Binafsi kukuza uchumi wa Nchi kupitia sekta ya Viwanda.

Imetolewa na;

Bi. Bengi Issa

Katibu Mtendaji,

15 Mei, 2019